# MPANGO WA MUNGU WA UPONYAJI

Watu wengi hawajapokea uponyaji wa Mungu kwa sababu hawana hakika kuwa ni mapenzi ya Mungu kuwaponya.
Wakati Yesu Kristo aliomba, “Mapenzi yako yatendeke duniani kama ilivyo mbinguni,” alimaanisha, “Enenda katika dunia hii  Baba, jinsi ufanyavyo mbinguni.” Mbinguni kulingana na Ufunuo 21:4, hakutakua na machozi, mauti, maombolezo wala kilio wala, maumivu. Hakutakuwa na magonjwa.
Ni muhimu sana kwetu kustawisha mapenzi ya Mungu na mpango wake wa uponyaji. Kisha tutaweza kupokea kupona kwa miili yetu. Hatuna budi kujua ukweli kuhusu mapenzi ya Mungu kwetu. Na tulitazame neno lake maana ndilo mapenzi yake. Tuweke kando tajriba yetu na ya wengi kuhusu uponyaji au kukosekana kwake na tuangalie Mungu alisemalo kuhusu uponyaji!
Katika Mwanzo 1-3 tunamwona mwanadamu akiumbwa kwa mfano wa Mungu. Ugonjwa ulikuwa jambo geni kwake. Magonjwa ni sehemu ya uozo wa kifo ambao pia haukua na nafasi katika uumbaji wa Mungu. “Mshahara wa dhambi ni mauti (kimwili na kiroho)” Mwanadamu alipoanguka dhambini, alianguka katika utumwa na kutekwa na Shetani kulingana na Yesu, “*Adui* (Shetani) *amekuja kuiba, kuchinja na kuharibu*.” (Yohana 10:10) Mwanaadamu akawa mwepesi wa kupatwa na magonjwa katika mwili wake kwa sababu Shetani sasa amekuja kuwa bwana wake.

MAGONJWA HAYATOKANI NA MUNGU.
*“Habari za Yesu wa Nazareti, jinsi Mungu alivyomtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu naye akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na Ibilisi, kwa maana Mungu alikuwa pamoja naye.* (Matendo ya Mitume)10:38)

“ *Na tazama, palikuwa na mwanamke aliyekuwa na pepo wa udhaifu muda wa miaka kumi na minane, naye amepindana, hawezi kujinyoosha kabisa. Yesu alipomwona alimwita, akamwambia, mama umefunguliwa katika udhaifu wako. Akaweka mikono juu yake, naye akanyoka mara hiyo, akamtukuza Mungu...” (Mstari 16,17) “ Na huyu mwanamke, aliye wa uzao wa Ibrahimu, ambaye Shetani amemfunga miaka kumi na minane hii, haikupasa afunguliwe kifungo hiki siku ya Sabato?...... mkutano wote wakafurahi kwa sababu ya mambo matukufu yaliyotendwa naye.”* (Luka 13:11-17)

Nguvu za Mungu zilitiririka kupitia kwa Yesu ili kutenda matendo ya Baba katika ulimwengu uliotawaliwa na Shetani. Nguvu na mapenzi ya Mungu ni kuwatoa watu kutoka kwa nyanyaso na utumwa wa shetani. Kama Yesu alivyoonyesha, magonjwa ni nyanyaso kutoka kwa Shetani. Kuugua hakumaanishi kuwa tumepagawa (kujawa na kutawaliwa na pepo) hata ikiwa magonjwa yanaweza tokana na kupagawa. Wakati mwingi magonjwa ni nyanyaso za Shetani akaivamai miili yetu au fikra zetu.

**Kwa nini Yesu alikuja?**

*“Roho wa Bwana yu juu yangu, kwa maana amenitia mafuta kuhubiria maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, na vipofu kupata kuona tena, kuwaacha huru waliosetwa. Na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliw*a. (Luka 4:18-19)

Yesu alikuja kutuweka huru sote kutokana na utumwa, nyanyaso na nguvu za Shetani. Shetani ni

mshinde kwa sababu Yesu amemfunga na kutupatia uwezo (amri) katika jinal lake kumfunga. Tazama Mathayo 12:28-30) na Mathayo 18:18, inayonena kuhusu kusamehe dhambi au kutosamehe dhambi, kufungua na kutofungua nguvu za Shetani)
Yesu akasema "*Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu, mimi nilikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele."* (Yohana 10:10)

**AGANO JIPYA**
Kama inavyodhihirika katika Agano la Kale, chini ya Agano hilo, Mungu aliahidi baraka kwa watu wake ikiwa wangemtii. (Tazama Kumbukumbu La Torati 7:11-15, 28:1-14 ) Wangemiliki kila kitu-ufanisi, utukufu, uzao wa nchi na uzao wa tumbo na angewaondolea ugonjwa wote wala hangetia juu yao maradhi yoyote mabaya wayajuayo ya Misri. (Kumbukumbu La Torati 7:15) Wakikosa kutii maagizo na amri za Mungu, kulikuwa na laana au adhabu zilizojumuisha umaskini, utasa, magonjwa, maradhi, kifo n.k.
Tatizo kubwa katika Agano la Kale ni kuwa hakuna yeyote angezifuata amri za Mungu kiamilifu. Mungu alitoa Agano Jipya (Ahadi) lililohusiana na Yesu Kristo.

*"Lakini sasa amepata* (Yesu) *huduma iliyo bora zaidi, kwa kadiri alivyo mjumbe wa Agano lilillo bora lililoamriwa juu ya ahadi zilizo bora,"* (Waebrania 8:6)

Mungu alifanya ahadi ya Agano Jipya na mwanadamu kwa misingi ya ahadi bora zaidi zilizotimizwa katika Yesu Kristo kwa ajili yetu.

"*Ni dhahiri ya kwamba hakuna mtu ahesabiwaye haki mbele za Mungu katika sheria; kwa sababu mwenye haki ataishi kwa imani na Torati haikuja kwa imani, bali ayatendaye hayo ataishi katika hayo. Kristo alitukomboa katika laana ya Torati, kwa kuwa alifanywa laana ya Torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu; maana imeandikwa, amelaaniwa kila mtu aangikwaye juu ya mti ili kwamba baraka ya Ibrahimu iwafikie mataifa katika Yesu Kristo, tupate kupokea ahadi ya Roho kwa njia ya imani.* (Wagalatia 3:11-14)

Yesu masalabani alijitwika laana ya sheria (umaskini, kutenganishwa na Mungu, utasa, kifo na magonjwa) pahala petu akituweka huru kupokea baraka za Mungu.(ufanisi, kuunganishwa na Mungu, kuondolewa utasa, kukarimiwa uzima na uhai) kwa imani. Tunazipokea baraka hizi zote kama urithi wetu kwa imani katika Kristo.

Mungu ametupa nafasi tujiamulie tulitakalo.

Katika Agano la Kale Mungu alisema, "*Nazishuhudiza mbingu na nchi juu yenu hivi leo, kuwa nimekuwekea mbele yako, uzima na mauti, baraka na laana, basi chagua uzima."*
(Kumbukumbu la Torati 30:19-20) kuchagua baraka na uzima kulikuwa ni kuchagua kuzitii sheria za Mungu. Mungu anataka tupate baraka zake zote.

Katika Agano Jipya tumekarimiwa baraka za Mungu kupitia kifo na kufufuka kwa Yesu. Kuchagua baraka na uzima ni kuchagua kuzipokea kwa imani katika Yesu Kristo. Mungu anataka tuwe na uzima wa milele, afya na baraka zingine zote (uzima tele) aliotukarimia katika Yesu Kristo. Tuchague kumpokea Yesu kwa imani au tuchague kumkataa, tujihukumu wenyewe na kujitenga na baraka za

Mungu. (Yohana 3:15-21) Afya ni sehemu ya baraka zetu katika Yesu.
“ *Hakika ameyajchukua masikitiko yetu. Ametijwita huzuni zetu; lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, amepigwa na Mungu na kuteswa. Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichumbuliwa kwa maovu yetu. Adhabu ya imani yetu ilikuwa juu yake na kwa kupigwa kwake sisi tumepona*. (Isaya 53:4-5)

Ukiyangalia baadhi ya maneno katika kamusi ya Kiebrania, utapata kile Yesu alichotutimizia pale msalabani. Mistari hii hutumiwa kuonyesha kuwa Yesu alituondolea dhambi zetu pale masalabani. Hata hivyo Yesu alitutimizia mengine mengi.

Kulingana na kamusi ya Strong, maana ya maneno yafuatayo katika lugha ya Kiebrania ni:

Masikitiko- kutokuwa na afya, magonjwa, hofu na maradhi (mstari wa 4)
Huzuni- majonzi, kuteswa, masikitiko, maumivu, maombolezo.
Kuponya- kutibu, kuponya kama daktari, tabibu, kupa uzima. (mstari wa 5)

(Tanbihi:Mstari huu hausemi tumwendee daktari ili tupone lakini tumeponywa kwa kupigwa kwake) Yesu. Alituweka huru kabisa kutoka kwa utumwa wa Shetani, dhambi zetu, kifo, kutokuwa na afya, magonjwa, hofu, maradhi, majonzi, kuteswa, masikitiko/ maombolezo, maumivu na huzuni. Yesu alituponya roho, akili na mwili.

Kwetu sisi tunaomwamini Yesu Kristo, tunaweza kushi hapa duniani kama mbinguni kwa imani yake ndani ya sala yake ilhali mambo mengine yanaendelea katika ulimwengu unaotuzungira. Hata hivyo hatuna haja ya kuwa nayo kwa sababu ndani ya Kristo tuko “ *katika ulimwengu, lakini sisi si wa ulimwengu.”* (Yohana 17:14-17) Nguvu za Kristo zinaishi ndani yetui na aliomba Baba kuwa tulindwe na yule mwovu.

*“Hata kulipokuwa jioni, wakamletea wengi wenye pepo, akawatoa pepo kwa neno lake, akawaponya wote waliokuwa hawawezi, ili litimie lile neno lilionenwa na nabii Isaya, akasema, mwenyewe aliutwaa udhaifu wetu, na kuyachukua magonjwa yetu.* (Mathayo 8:16-17)

“*Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu wa mambo ya dhambi tuwe hai kwa mambo ya haki, na kwa kupigwa kwake mliponywa.*” (1 Petro 2:24)

“*Kwa maana rahisi ni lipi, ni kusema, umesamehewa dhambi zako, au ni kusema, ondoka, uende? Lakini mpate kujua ya kwamba mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi, (anamwambia mwenye kupooza) ondoka, ujitwike kitanda chako, ujendee nyumbani kwako. Akaondoka akaenda zake nyumabni kwake.*” (Mathayo 9:5-7)

Yesu anaonyesha kuwa kusamehewa dhambi na kupona kwa mwili na akili huandamana na kuwa na nguvu za kutenda yote mawili.

Kwa wale wetu wanomwamini Mungu na neno lake kabisa, bila shaka tunaona kuwa ameipatia Kanisa lake huduma hii ya uponyaji. Tunaenda katika jina la Yesu, tukitangaza Injili(habari njema) kuwa

ametuweka huru, roho akili na mwili kutokana na kuakandamizwa na Shetani.hivi ndivyo Mungu asemavyo,tunaweza kupokea na kuamini au kutopokea na kutoamini.Na sababu kuwa sisi hatuamini hivi haimanishi kuwa Mungu ni mwongo. Sababu kuwa sisi hatuamini haimanishi kuwa Mungu hawezi kutenda tukiamini.Leo kote katika ulimwengu huu Mungu anawaponya wale wote wanaoamini neno lake
Yesu hakufanya miujiza mingi huko Nazareti kwa sababu ya kutoamini kwa watu(Mathayo 13:58) Tusiachilie kutoamini kuwe katikati yetu katika makanisa yetu au nyoyoni mwetu.Makanisa nayawafunze watu wa Mungu kuamini alisemalo Mungu na kile anachosema ni chetu katika Yesu Kristo(Injili)

Yesu akasema ,'*Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.Aaminiye na kubatizwa ataokoka asiyeamini atahukumiwa.Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio;kwa jina langu watatoa pepo,watasema kwa lugha mpya,watashika nyoka, hata wakinywa kitu cha kufisha,hakitawadhuru kabisa,wataweka mikono yao juu ya wagonjwa,nao watapata afya'(Mariko16;15-18)*

*'Mtu wa kwenu amekuwa hawezi(mgonjwa)?Na awaite wazee wa kanisa;nao wamwombee,na kumpaka mafuta* kwa jina la Bwana.Na kule kuomba kwa imani kutamwokoa(Neno hili la kigiriki linamaanisha kuokoa,kukomboa au kulinda, kuponya ,kuhifadhi,kuokoa(nafsi) ,fanya vizuri,fanya mzima) *mgonjwa yule.Na Bwana atamwinua,hata ikawa amefanya dhambi atasamehewa.Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi na kuombeana,mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana,akiomba kwa bidii(*Yakobo5;14-16)

Kifungu hiki kinawahusu waaminio nasi ndio waaminio hao waliofanyika haki ya Mungu katika Kristo.Mungu atainua,kuponya,na kusamehe wote wanaotaka kuponywa na kusamehewa katika msingi wa neno lake tukiamini tunapoomba.

Yesu alisema,'*Mwaminini Mungu.Amin nanawaambia,yeyote atakayeuambia mlima huu ng'oka ukatupwe baharini ,wala asione shaka moyoni mwake,ila aamini kwamba hayo asemayo yametukia,yatakuwa yake,kwa sababu hiyo nawaambia,yoyote myaombayo mkisali amini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu*(Mariko 11;22-24)

*'Amini,amini ,nawaambieni,yeye aaminiye mimi,kazi nizifanyazo mimi yeye naye atazifanya,naam, na kubwa kuliko hizo atafanya,kwa kuwa mimi naenda kwa Baba.Nanyi mkiomba lolote kwa jina langu, hilo nitalifanya,ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana.Mkiniomba neno lolote kwa jina langu nitalifanya*(Yohana 14;12-140)

Kuna wale wenye karama za uponyaji katika Roho Mtakatifu.Hata hivyo vifungu hivi huwahusu wale waaminio katika Kristo.Tunatakiwa kuomba,kuwaweka watu mikono na kutarajia Mungu kuwaponya.Huenda tusione matokeo wakati uo huo, lakini mtu ataupokea uponyaji.(katika roho,uponyaji hutokea wakati tunapolinena neno la Mungu kisha utadhihiri katika awamu ya kimwili)

Ni mpenzi ya Mungu kuponya!Yesu aliwaponya wote waloletwa kwake.Huduma ya Yesu katika utiifu wa uliokamilika kwa Babake.

“K*wa kuamini mimi sikushuka kutoka mbinguni ili nifanye mapenzi yangu ,bali mapenzi yake aliyenipeleka(aliyenituma)”(Yohana 6;380)'Mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote,wewe usinijue,Filipo?Aliyeniona mimi amemwona Baba;basi wewe wasemaje,utuonyeshe Baba?Husadiki ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani yangu?Hayo maneno niwaambiayo mimi siyasemi kwa shauri langu,lakini kwa Baba akaaye ndani ya yangu huzifanya kazi zake(Yohana 14;9-10)*

Yesu alisema kuwa Baba alifanya uponyaji wote huu na matendo makuu kupitia kwake,Ni mapenzi ya Mungu kumponya yeyote anayemtafuta (Tazama Matendo ya Mitume 10;38 Mathayo 4;23-24,Mathayo 8;16-17,Mathayo 9;35,Mathayo 10;1,12;15,14;14,14;34-36,Luka 4;40,Matendo ya Mitume 5;16)

Tunaweza kuamini Mungu anaweza au tayari ametuponya(1Petro 2;24),au tusiamini anaweza kutuponya.Kutoweza au magonjwa hayafai kuishi ndani ya miili yetu kwa sababu tu watoto wa Mungu ndani ya Yesu Kristo.Ni jambo la kushangaza vile watu wanaweza kuamini kuwa wamesamehewa dhambi zao ilhali hawaamini Yesu anaponya.Tunajuaje ni mapenzi ya Mungu tuokolewe?-kulingana na neno la Mungu.Tunajuaje ni mapenzi ya Mungu tupone?-kulingana na neno la Mungu.Ikiwa Mungu hataki tuokolewe au tupone, kwa nini tujisumbue kuombea wokovu au uponyaji?Tutakuwa tukipoteza muda wetu.

Mungu hapendelei(Matendo ya Mitume 10;34-38,Warumi2;11,Waefeso 6;9, Wakolosai3;25)Anataka watu wote wapate wokovu na uponyaji kwa maana mambo haya mawili huandamana kulingana na neno la Mungu.

Pengine unawaza “Kwa nini si kila mtu anapona?'Kuna sababu sawa na hii, si kila mtu anayeupokea wokovu.Kuna baadhi ya watu wanaochagua kuwa wagonjwa.Baadhi ya watu hakika hawataki kuponywa. Baadhi ya watu hawaamini kuwa Mungu atawaponya.Wengine hawajui ahadi na neno la Mungu kuhusu mapenzi yake na urithi wao katika Kristo.

**Dhana potovu kuhusu magonjwa.**

1. **Magonjwa hutokana na dhambi.**
Mara nyingi magonjwa hutokana na dhambi .Hofu, woga kuhukumika n.k, husababisha magonjwa hata hivyo, huu si ukweli kila wakati tupatapo magonjwa. kulingana na ahadi ya Mungu (Yakobo 5: 14- 15), hata ikiwa dhambi husababisha magonjwa, tunasamehewa wakati tunatubu na kupona wakati tunapoomba.

2. **Magonjwa humpa Mungu utukufu.**

Huu si ukweli . katika Injili na Matendo ya Mitume, Mungu aliupokea utukufu kila mara watu wake walipata kupona au kukombolewa. Mambo yatokanayo na Shetani hayamtukuzi Mungu. Mungu hupokea utukufu mtu akiwekwa huru kutoka utumwani mwa Shetani.

3. **Magonjwa hutokea wakati Mungu anatutakasa au kutuadhibu.**

Yesu alitukomboa katika laana au adhabu ya Torati - magonjwa yakiwemo. Mungu hatufundishi kutoenda barabarani kwa kutugonga kwa gari. Mungu haweki saratani au magonjwa ya moyo ndani

yetu ili tupate fundisho , hata ikiwa twapata fundisho tunapomtafuta Mungu katika hali kama hii. Mungu anaturudi kupitia neno lake. " N*inyi mmekwisha kuwa safi kwa sababu ya lile neno nililowaambia.*" (Yohana 15: 3) Hatuwavunji mikono watoto wetutunapowarudi. tunawaagiza. Mungu hutuagiza kwa neno lake." *Maana yeye ambaye Bwana ampendaye, humrudi. naye humpiga kila mwana amkubaliye*."(Waebrania 12:6) Neno "Kurudi" humaanisha "kulea mtoto, elimisha , adibu, agiza, funza.'

tunapolitii neno la Mungu, tunafichika ndani ya ulinzi wa Mungu na mwovu hawezi kutuguza.(1 Yohana 5: 18) . Hakuna magonjwa yanayoweza kuishi ndani yetu tena. hata hivyo, nikikosa kumtii Mungu, nachagua kujiondoa katika ulinzi wa Mungu ambapo Shetani anaweza kunidhuru.Mungu aliruhusu magonjwa kuwajia wale wasiomtii- wale waliotii hawakuugua. Yesu Kristo alitukomboa katika laana na adhabu ya kutotii sheria ya Mungu- magonjwa, umaskini na mauti ya pili. tumeadibika kwa neno la Mungu. Mungu hawezi kujaribiwa kwa uovu. tunaweza kuyakataa magonjwa yajaribiyayo kutujia kutokana na Shetani.Magonjwa yatokanayo na dhambi au kuidhuru miili yetu kwa kuifanyiza kazi kupita kiasi, kutenda lolote tulitakalo au mitazamo mibaya yaweza kuponywa tunapotubu dhambi zetu na kupokea msamaha wa Mungu, uponyaji na nguvu za kuyazuia majaribu yanayoleta magonjwa.

4. **<u>Magonjwa hutokana na ukosefu wa imani.</u>**

Huu si ukweli kabisa Ni kweli kuwa watu wengi hawaamini katika kukataa magonjwa au katika uponyaji wa Mungu .Hata hivyo mara nyingi watu huugua kwa sababu ya kukosa kujua kuwa ni mapenzi yaMungu wapone na wakarimiwa nguvu za Mungu za uponyaji. Wanatakiwa watafute na kutafakari ahadi ya Mungu wakijua kuwa tayari wamekarimiwa uponyaji katika Yesu Kristo kulimgana na neno la Mungu.

Na Ayubu je? Ayubu alipata maafa yake yote kwa mkono wa Shetani. Lakini Mungu hukuruhusu? Naam, Mungu hangefanya chochote. Ayubu alichagua kuenenda kwa woga kuliuko kuenenda kwa imani. " *Maana jambo hilo nichalo hunipata, nalo linitialo hofu hunijilia."* (Ayubu 3: 25) Ayubu sababu ya woga wake alifungulia uvamizi na kutekwa na Shetani kwa miezi tisa wala si maisha yake yote,Lakini katika sura ya 42, Ayubu alipotubu na kuwaombea marafiki zake baraka; " kisha BWANA akageuliza uteka wa Ayubu, hapo alipowaombea rafiki zake; BWANA naye akampa Ayubu mara mbili kuliko hayo aliyokuwa nayo kwanza (Ayubu 42:10), *Mungu alimponya Ayubu na kumpa utajiri maradufu kuliko aliyokuwa nayo awali na kumkomboa utumwani mwa Shetani. kisha baada ya mambo hayo Ayubu akaishi miaka mia na arobaini........Basi Ayubu akafa, mzee sana mwenye kujawa na siku.* (Ayubu 42: 16- 17)

Je na mwiba wa Paulo ( 2 Wakorintho 12: 7- 9)? Neno la Mungu lasema "*Mwiba*" ni pepo au mjumbe wa Shetani wala si magonjwa au maradhi.( mstari 7)

Kunao wanaofikiria kuwa *mwiba* huu ulikuwa udhaifu katika mwili au ulemavu. (Tazama Wagalatia 4: 13-14) Tunza: Galatia ndipo pahali pa kwanza Paulo kutia nanga baada ya kuondoka Listra). Hata hivyo naonelea kuwa kuna uwezekano wakati *"Mwiba"* wa Paulo ( mjumbe wa Shetani) alipozua mateso (adha) Paulo alipigwa kwa mawe huko Listra. (Matendo ya Mitume 14: 19-22) Matokeo ya mateso hayo yalikuwa ni adha.*Mwiba* huu hata hivyo ulikuwa mjumbe wa Shetani wala si maradhi au ugonjwa. tunajua Paulo alionyeshwa na Yesu yalivyo mengi ambayo yangempasa kuteswa kwa ajili ya

jina lake (Matendo ya Mitume 9: 16) Popote alipoenda alivamiwa na Shetani kupitia watu na kuteseka sana.

Katika Yoshua 23: 13 Mungu alikimwambia Yoshua ya kuwa ikiwa Waisraeli hawataendelea kumpenda Mungu, watu wa Kanani watakuwa *mwiba* machoni mwao na mbavuni mwao. (Jambo hili pia linapatikana katika Hesabu 33:55 na Ezekieli 28:24). Katika orodha ya Paulo ya mambo aliyoyapitia hakuna magonjwa yoyote yaliyotajwa, lakini yote aliyoyapitia yalihusiana na mateso kwa ajili ya Kristo. (2 Wakorintho 6: 4- 10; 11: 23-27).

Mungu hangemwondoa mjumbe wa Shetani, *mwiba* wa Paulo, kwa sababu siku ya Shetani haijawadia mpaka Kristo arudi. Paulo alikuwa akiomba Shetani aondolewe. Mungu hangeweza kulijibu lile ombi hadi wakati wake utimie.Hata hivyo, Mungu alimpa Paulo (na hutupa nasi) neema (nguvu) itoshayo kumshinda mwovu Shetani, *"Mpigeni Shetani naye atawakimbia*" (Yakobo 4:7).

Hatuwezi kutumia *mwiba* wa Paulo kama sababu ya kuvumilia magonjwa kwa sababu hakuna hakikisho kuwa mwiba huo ulikuwa ugonjwa.Tusiutumie *mwiba* huu kama sababu ya kutoamini. Mapenzi na tamanio la Mungu ni tupate afya na uponya. Yesu aliye mfano wetu, hajawahi kuugua.

Nini kiponyacho? Neno la Mungu huponya......Imani yetu katika neno la Mungu ndio njia ya kupokea uponyaji.

" *Hulituma neno lake huwaponya, huwatoa katika maangamizo yao."* (Zaburi 107: 20)

*"Mwanangu, sikiliza maneno yangu; tega sikio lako, uzisikie kauli zangu. zisiondoke machoni pako; uzihifadhi ndani ya moyo wako. maana ni uhai kwa wale wazipatao na afya ya mwili wao wote.* (Mithali 4: 20-22)

JINSI YA KUPOKEA UPONYAJI.
1. Tamani kupona
2.Tamani neno la Mungu kukuhusu
3.Liamini
4. Omba kulingana na neno la Mungu.
5.Mshukuru Mungu kwa kupokea uponyaji wako (Mariko 11: 24)
6. Kiri vile neno lsa Mungu lisemavyo wala si vile unavyoona au kuhisi. "*Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarjiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.* " (Waebrania 11:1) Imani yako katika neno la Mungu ndiyo hakika na bayana( dhihirisho) ya uponya wako hadi idhihiri katika mwili wako. Kulingana na neno la Mungu utauona: uponya wako sifu na kutukuza Mungu! Endelea kumshukuru na kumsifu kuwa kwa kupigwa kwa Yesu umepona.
7. Dhihirisha kupona kwako. fanya kile hukuwa ukifanya awali

**NENO LA MUNGU KUHUSU UPONYAJI**
Uponyaji................katika upatanisho/suluhu.

"*Hakika ameyachukua masikitiko yetu,*(maana yake dhahiri katika lugha ya kiebrania ni magonjwa). a*mejitwika huzuni zetu;* (maumivu), *lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, amepigiwa na Mungu, na*

*kuteswa.Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu,alichumbuliwa kwa maovu yetu,adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi nimepona* (Isaya 53:4-5)

"*..Naye ......akawaponya wote waliokuwa hawawezi (wagonjwa), ili litimie lile neno lililonenwa na nabii Isaya akisema, mwenyewe aliutwaa udhaifu wetu na kuyachukua magonjwa yetu."* Mathayo 8: 16- 17)

" *Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa kwake mliponywa,'* (IPetro 2:24)

" *Kristo alitukomboa katika ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu; maana imeandikwa, ameelaaniwa kila mtu aangikwaye juu ya mti* (Wagalatia 3:13)

Kulingana na kumbukumbu la Tarati 28: 15-22, 27-29, 35 -61, magonjwa na maradhi yote ni laana ya torati . lakini sifu Mungu kulingana na Wagalatia 3:13, kristo ametukomboa katika laana ya torati!

Uponyaji...............mapenzi ya Baba.

"*...............Kwa kuwa mimi ndimi BWANA nikuponyaye*."

"*Nanyi mtamtumikia BWANA, Mungu wenu, naye atakibarikia chkula chako, na maji yako; nami nitakuondolea ugonjwa kati yako; hapatakuwa na mwenye kuharibu mimba wala aliye tasa , katika nchi yako na hesabu ya siku zako nitaitimiza* (Kutoka 23:25-26)

*"Kwa maana macho ya BWANA hukimbia -kimbia duniani mwote, ili ajionyeshe mwenye nguvu kwa ajili ya hao waliokamilika moyo kuelekea kwake*. (Mambo ya Nyakati 16: 9)

" *Mabaya hayatakupata wewe, wala tauni hitaikaribia hema yako; kwa siku nyingi nitamshibisha , nami niyamwonyesha wokovu wangu,'* (Zaburi 91: 10, 16)

*"Ewe nafsi yangu, umuhimidi BWANA, wala usizisahau Fadhili zake zote. akusamehe maovu yako yote, akuponya magonjwa yako yote.*" (Zaburi 103: 2-3)

" *Hulituma neno lake, huwaponya...........*" (Zaburi 107:20)

*"Ndivyo litakavyokuwa neno langu, litokalo katika kinywa changu; halitanirundia bure, bali litatimiza mapenzi yangu , nalo litafanikiwa katika mambo yale niliyolituma,*"(Isaya 55:11)

" *Basi ikiwa ninyi mlio waovu, mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema je! si zaidi sana Baba yenu aliye mbinguni atawapa mema wao waomwombao*?" (Mathayo 7:11)

" *Kila kutoa kuliko kwema, na kila kitolewacho kilicho kamili, hutoka juu, hushuka kwa Baba wa mianga..........*" (Yakobo 1:17)

*" Na tazama, akaja mtu mwenye ukoma akamsujudia, akisema, Bwana, ukitaka, waweza kunitakasa.*

*Yesu akanyosha mkono, akamgusa, akisema nataka; takasika*." (Mathayo 8:2-3)

*Yesu alinena kuhusu, kwa kuwa mimi sikushuka kutoka mbunguni ili nifanye mapenzi yangu bali mapenzi yake aliyenituma."* (Yohana 6: 38)

Chochote alichokitenda Yesu alipokuwa hapa duniani kilikuwa mapenzi ya Baba. alikuwa mapenzi ya Baba kwenye matendo . ukitaka kujua mapenzi ya
Baba, mtazame Yesu.

Uponyanji..........matendo ya Yesu.

*" Habari za Yesu wa Nazareti, jinzi Mungu alivyyomtia mafuta kwa Roho mtakatifu na nguvu akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na Ibilisi; kwa maana Mungu alikuwa pamoja naye*."( Matendo ya Mitume 10:38)

Ukweli huu ukae ndani ya moyo wako: Kristo ni mponya, Shetani ni dhalimu." *Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu; mimi nalikuja ili wawe na uzima , kisha wawe nao tele*." (Yohana 109:10)

*" Naye Yesu alikuwa akizunguka katika miji yote na vijiji , akifundisha,....... na kuhubiri... na kuponya magonjwa yote na udhaifu wa kila aina."* (Mathayo 9:35)

" *Wakamwendea makutano mengi wakamletea viwete, vipovu, mabubu, vilema na wengine wengi, wakawaweka miguuni pake; akawaponya; hata ule mkutano wakastaajabu, walipowaona mabubu wanasema, vilema wanakuwa wazima, viwete wanakwenda, na vipofu wanaona; wakamtukuza Mungu wa Israeli.* (Mathayo 15: 30-31)

"*Yesu Kristo ni yeye yule, jana leo na hata milele.*'(Waebrania 13:8)

Uponyaji....................huduma ya kanisa.

"*Amin,amin, nawaambieni, yeye aniaminiye mimi , kazi nizifanyazo mimi, naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba.*" (Yohana 14:12)

" *Akawaambia , endeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe....... Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo.......wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya.*" (Mariko 16: 15, 17 - 18)

"*Mtu wa kwenu amekuwa hawezi? Na awaite wazee wa kanisa ; nao wamwombee, na kumpaka mafuta kwa jina la Bwana . na kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgoinjwa yule, na Bwana atamwinua; hata ikiwa amefanya dhambi, atasamchewa*."(Yakobo 5: 14- 15)

*"Mpenzi naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya yako, kama vile roho yako ifanikiwavyo.*"(3Yohana 1:2)

Uponyaji........Mungu akifanya kazi ndani yetu.

" *Ninyi watoto wadogo , mwatokana na Mungu nanyi mmewashinda, kwa sababu yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia.*" (1 Yohana 4:4)

..........Imani katika uponyaji

"*Amin, nawaambia, yeyote atakayeuambia mlima huu, ng'oka ukatupwe baharini, wala asione shaka moyoni mwake, ila aamini kwamba hayo asemayo yametukia, yatakuwa yake.*" (Mariko 11: 23)

.............ombi la imani.

"*Kwa sababu hiyo nawaambia, yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.*" (Mariko 11:24)

© 1985, Dr. Randy Brodhagen, Glory To God Ministries International™,
all rights reserved,
www.glorytogod.org